

# KUHUSU SISI

NPCC ni kituo cha  
Kitaalamu  
kilichoanzishwa kwa  
Sheria ya Mamlaka  
ya Maabara  
ya Mkemia Mkuu wa  
Serikali, Na 8 ya  
Mwaka 2016 ili kutoa  
huduma za udhibiti  
wa matukio ya sumu  
nchini.



## WASILIANA NASI

0800112031 Masaa 24  
022 222 1410 Muda wa Kazi



5 Barack Obama Drive  
Dsr es Salaam

**MAMLAKA YA  
MAABARA YA MKEMIA  
MKUU WA SERIKALI  
KITUO CHA TAIFA CHA  
KUDHIBITI MATUKIO  
YA SUMU**



## Sumu maana yake nini?

---

Sumu ni kitu chochote ambacho kinaweza kudhuru mwili wako. Inaweza ikawa kwa njia ya kuvuta hewa, kumeza/kula kugusa (njia ya ngozi) au kuchomwa sindano.

Sumu inaweza kumpata mtu:

- Ama kama ajali
- Ama Makusudi (kwa kuamua yeye mwenyewe au mtu/watu wengine)

---

### Namna tunavyokumbana na sumu

#### **KWA KUVUTA HEWA**

Kwa kuvuta hewa yenye sumu, matonetone, mvuke ukungu, au vumbi hutengeneza sumu ambayo hunyonyea kupitia utando uliopo mdomoni, kooni na mapafu kwa kufanya uharibifu

#### **KWA KUMEZA AU KULA**

Mfano Kemikali nyingi zitumikazo Maabara nihatari sana ziingiapo mdomoni na zikimezwa

#### **KWA KUGUSA NGOZI NA MACHO**

Kugusa ngozi mara nyingi imepelekea kukumbwa na sumu ya kemikali. Taarifa humwendea mgonjwa kwa kuwashwa ngozi lakini vitu vingi hufiyonzwa kupitia ngozi

#### **KWA NJIA YA SINDANO**

Sumu kwa njia hii ni mara chache sana kutokea, lakini uwezekano upo kwa watumiaji dawa za kulevya au kosa la kitabibu

---

### Sumu inasababishwa na vitu gani?

Kuna vitu mbali mbali ambavyo ni hatarishi na vinasababisha sumu Navyo ni:

- Kemikali ya kuondolea rangi za kucha,
- Kemikali za kusukutua mdomo ambazo ni hatarishikwa watoto
- Kemikali za kusafishia sakafu na vitakatishi
- Rangi na "thinner"
- Viutilifu au viuavisumbufu
- Mbolea hususani za viwandani na Kemikali za kuua fangasi
- Metali, kama vile Risasi, Zebaki na Kemikali zisizo metali
- Dawa zitolewazo hospitalini na zile zinunuliwazo kutoka maduka ya dawa zinapo changanywa au kutumiwa vibaya
- Dawa za Kienyeji
- Madawa ya kulevya
- Pombe
- Hewa ya ukaa
- Vyakula vilivyo haribika/ kuharibiwa "Spoiled food"
- Mimea (kama vile uyoga, maua,)
- Sumu itokanayo na kuumwa na nyoka au wadudu

#### **Dalili kwa aliyekumbwa na sumu**

---

Madhara ya sumu hutegemea na kisababishi, kiasi chake, na namna kilivyo mkumba mwathiriwa. Umri wake, uzito, na hali yake ya kiafya vyote vitakuwa na mchango wa dalili.

Dalili zifuatazo mara nyingi hutokea:

- Kichefuchefu na/au kutapika
- Kuharisha/kuhara
- Vipele
- Wekundu au michubuko kwenye mdomo
- Midomo kukauka
- Kujaa mate mdomoni au kutokwa na mapovu mdomoni
- Kupumua kwa shida
- Kuvimba au kusinyaa mboni ya jicho
- Kuchanganyikiwa
- Kuishiwa nguvu
- Kutetemeka au kupoteza fahamu

#### **Kwa Dharura na Msaada**

**Piga Simu ya Bure:**

**0800112031**